WIZARA YA NISHATI

# NewsBulletin

HABARI ZA NISHATI

Toleo Namba 70 | Sept 1 - 30 2025



# VITUO VYA CNG VYAONDOLEWA VAT

WIZARA YA NISHATI

# BODI YA UHARIRI


**MWENYEKITI**

Mhandisi Felchesmi Mramba

**MAKAMU MWENYEKITI**

Dkt. James Mataragio

**MHARIRI**

Neema Chalila Mbuja
Teresia Mhagama

**WAANDISHI**

Timotheo Mathayo
Zuwena Msuya
Felista Charles
Petro Mwanda
Judith Hasani

**WAPIGA PICHA**

Henry Kilasila
Godfrey Mwemezi
Ruben Richard
Amanzi Kimonjo

**MSANIFU KURASA**

Brian Mbaga

© NISHATI 2025


Hamilton Beach
45

# NISHATI SAFI YA KUPIKIA
# OKOA MAISHA NA MAZINGIRA



# SERIKALI YAONDOA VAT KWA VITUO VYA GESI ASILIA ILIYOSHINDILIWA (CNG)

- Lengo ni kuongeza uwanda wa matumizi ya CNG katika vyombo vya moto nchini
- Mhandisi Mramba azindua kituo cha Gesi Asilia iliyoshindiliwa ( CNG) cha PUMA Energy
- Asema vifaa vya kuwekea mifumo ya gesi kwenye vyombo vya moto pia imeondolewa
- Apongeza PUMA Energy kwa kuiunga mkono Serikali katika ujenzi wa vituo vya CNG



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba akijaza gesi asilia kwenye moja ya Chombo cha usafiri Maarufu kwa Bajaji Jijini Dar es salaam.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba amesema Serikali imeondoa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa vituo vyote vya Gesi iliyoshindiliwa (CNG) nchini ili kuhamasisha matumizi ya gesi asilia kwenye vyombo vya moto kupitia uwepo wa vituo vingi vya kutoa huduma hiyo kwa wananchi.

Amesema kuwa Serikali pia imeondoa kodi kwenye vifaa vya kuwekea mifumo hiyo ya gesi kwenye vyombo vya moto kama vile magari na bajaji ikiwa ni hatua pia ya kuhamasisha matumizi ya gesi asilia katika vyombo vya moto.

Mhandisi Mramba ameeleza hayo jijini Dar es Salaam wakati akizindua kituo cha Gesi Asilia iliyoshindiliwa (CNG) cha kampuni ya Puma Energy kilichopo Bagamoyo road.

“ Serikali inafanya jitihada hizi ili kutoa nafasi kwa watanzania kutumia gesi kwenye vyombo vyao vya moto kwa kurahisisha mazingira ya upatikanaji wake na pia kwa kuwa kuna unafuu wa gharama pale unapotumia Gesi Asilia ikilinganishwa na mafuta”. Amesema Mramba




Picha ya Pamoja ya viongozi na wadau mbalimbali katika uzinduzi wa kituo cha Gesi Asilia iliyoshindiliwa (CNG) cha kampuni ya Puma Energy kilichopo Bagamoyo road Jijini Dar Es salaam.

Mramba amesema kwa sasa kuna vituo 11 vya kujaza gesi kwenye magari jijini Dar es Salaam ambapo Serikali imedhamiria kuwa hadi ifikapo mwishoni mwa mwaka huu idadi ya vituo hivyo itakuwa imeongezeka na kufika 18 katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam.

Aidha, ameeleza kuwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limeshaleta magari sita yatakayokuwa yanazunguka kujaza gesi kwenye magari katika maeneo mbalimbali.

Katika hatua nyingine Mha. Mramba ameipongeza PUMA kwa ujenzi wa kituo hicho na kutoa wito kwa wadau mbalimbali kuendelea kuwekeza katika vituo hivyo vya CNG.

"Natoa wito pia kwa Wananchi na watumiaji wa vyombo vya moto kuweza kutumia gesi asilia kwani vituo vimeongezeka nchini na hivyo kupelekea huduma kuwa karibu na jamii zetu". Amesisitiza Mha. Mramba

Kwa upande wake, Bi. Fatma Abdallah ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Puma Energy amesema kampuni hiyo imejenga kituo hicho ili kuunga mkono juhudi za Serikali katika mageuzi ya matumizi ya nishati ambayo ni safi na salama katika kuendesha vyombo vya moto.

# MHANDISI MRAMBA NA JICA WAJADILI UTEKELEZAJI WA MIRADI YA NISHATI

- Ni wa usafirishaji umeme kutoka Tanzania hadi Uganda na Dodoma ring circuit
- Awasisitiza JICA kuwajengea uwezo wataalam wazawa katika usanifu wa mitandao ya usambazaji Gesi Asilia

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba amekutana na Wataalam kutoka Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) ili kujadili hali ya utekelezaji wa miradi ya Nishati inayofadhiliwa na shirika hilo kwa lengo la kuhakikisha kuwa miradi hiyo inatekelezwa kwa wakati na kwa ufanisi.



Picha ya Pamoja ya viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati na JICA (Japan International Cooperation Agency) mara baada ya kikao hicho kilichofanyika Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma.

Kikao hicho kimefanyika katika ofisi za Wizara ya Nishati Mtumba Jijini Dodoma ambapo pande hizo mbili pia zilijadiliana kuhusu suala la kujengea uwezo wataalam wa Wizara ya Nishati, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) katika masuala ya kusanifu mitandao ya usambazaji wa Gesi Asilia.

Miradi iliyojadiliwa kwa kina katika kikao hicho ni wa kusafirisha umeme kutoka Tanzania hadi Uganda (UTIP) na mradi wa umeme Dodoma Ring Circuit unaolenga kuzidi kuimarisha hali ya upatikanaji umeme Dodoma.

Katika kikao hicho, Mha. Mramba ameisisitiza JICA kuhusu suala la utekelezaji mradi wa mfano wa usambazaji gesi asilia katika Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma ambao utakuwa kielelezo cha manufaa ya gesi asilia iliyogunduliwa hapa nchini ambayo itasaidia pia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Vilevile, Mramba ameishukuru JICA kwa kufadhili miradi ya Nishati ambayo imekuwa chachu ya maendeleo nchini hususan katika Jiji la Dodoma ambalo linaendelea kukua kwa kasi.

# KATIBU MKUU MRAMBA AKUTANA NA KAMPUNI YA NYUKLIA YA CHINA

- Wajadili ushirikiano katika kuzalisha umeme wa nyuklia nchini
- Watanzania kujengewa uwezo katika masuala ya nyuklia




Viongozi mbalimbali katika picha ya Pamoja katika kikao kilichofanyika jijini Vienna, Austria pembezoni mwa Mkutano Mkuu wa 69 Wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomi (IAEA).

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba ameongoza ujumbe wa Serikali ya Tanzania katika kikao na Shirika la Taifa la Nyuklia la China (China National Nuclear Corporation – CNNC), kujadili fursa za ushirikiano katika kuanzisha na kuendeleza mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia teknolojia ya nyuklia.

Katika kikao kilichofanyika jijini Vienna, Austria pembezoni mwa Mkutano Mkuu wa 69 Wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomi (IAEA), Wawakilishi wa CNNC waliieleza Tanzania kuwa kampuni hiyo ina uzoefu mkubwa katika kujenga na kuendesha mitambo ya kuzalisha umeme wa nyuklia, na wako tayari kushirikiana na Tanzania katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi ya aina hiyo.

"Tanzania imeanza maandalizi ya kuzalisha umeme kwa kutumia nyuklia ikiwa ni utekelezaji wa dhamira na nia njema ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuona nchi inakuwa na vyanzo endelevu, salama na vya uhakika vya nishati, hivyo tupo tayari kushirikiana na CNNC katika safari hii ya kuzalisha umeme wa nyuklia." Amesema Mramba

Ametoa shukrani kwa CNNC kwa kuonesha nia ya kushirikiana na Tanzania, akibainisha kuwa Serikali ya Tanzania imeamua kuwekeza katika mradi wa kuzalisha umeme wa nyuklia kama sehemu ya mkakati wa kuongeza upatikanaji wa nishati endelevu na ya uhakika.

Katika kikao hicho, CNNC imeahidi kushirikiana na Tanzania katika kujenga uwezo wa kitaalamu kwa Watanzania kupitia mafunzo ya kiufundi, ziara za mafunzo, pamoja na kutoa ufadhili kwa masomo ya uzamili katika fani ya nyuklia. Hatua inayolenga kuhakikisha Tanzania inakuwa na wataalamu wa kutosha kusimamia na kuendeleza miradi ya nishati ya nyuklia nchini.

Kikao hicho kilihudhuriwa pia na Bw. Jing Zhang, Mkuu wa Idara ya Ufundi wa IAEA, Mha. Joseph Kirangi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Maji na Madini kutoka Zanzibar, Prof. Najat Mohamed, Mkurugenzi Mkuu wa Kamisheni ya Nguvu za Atomi Tanzania (TAEC), Mha Innocent Luoga, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu na Wataalam wa masuala ya Nyuklia.

# MHANDISI MRAMBA ASHIRIKI MKUTANO WA KIMATAIFA WA NGUVU ZA ATOMIKI NCHINI AUSTRIA

- Tanzania kupata uzoefu wa uzalishaji umeme kwa nyuklia
- Agizo la Rais Samia la uzalishaji umeme wa uranium laendelea kutekelezwa na Wizara ya Nishati

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mha.Felchesmi Mramba ameshiriki mkutano wa 69 wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki -IAEA jijini Vienna Austria ambao unawashirikisha wadau mbalimbali wanaotumia nishati ya nyuklia kama chanzo cha umeme.

Mha. Mramba ameshiriki mkutano huo wa kimataifa unaowakutanisha wadau mbalimbali na mataifa makubwa yanayotumia nyuklia kama chanzo kimojawapo cha kuzalisha umeme.

Mkutano huo unakuja kipindi ambacho Wizara ya Nishati imepewa jukumu kubwa na Raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan, la kuhakikiaha TANESCO inaaza kuzalisha umeme kwa kutumia madini ya Uranium yanayopatikana Namtumbo mkoa wa Ruvuma.

Tanzania inatarajia kutumia vema fursa ya mkutano huo wa 69 wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki kujifunza na kubadilishana uzoefu wa namna ya kuzalisha umeme kwa nguvu ya nyuklia ,pamoja na kuangalia fursa za uwekezaji kwenye miradi ya umeme .

Ujumbe wa Tanzania unaongozwa pia na Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof.



Viongozi mbalimbali katika mkutano wa 69 wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki -IAEA jijini Vienna Austria ambapo washiriki ni wadau mbalimbali wanaotumia nishati ya nyuklia kama chanzo cha umeme.

Carolyne Nombo.

Wajumbe Wengine walioshiriki Mkutano huo ni pamoja na Balozi wa Tanzania na Mwakilishi wa Kudumu Nchini Austria, Mhe. Naimi S. H. Aziz, Mha. Joseph John Kirangi Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Maji na Ardhi ya Zanzibar, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu kutoka Wizara ya Nishati Mha. Innocent Luoga pamoja na Viongozi Waandamizi na Wataalam kutoka Kamisheni ya Nguvu za Atomi (TAEC).

# RUZUKU YA SHILINGI MILIONI 250 YATOLEWA KWA WABUNIFU WA MATUMIZI BORA YA NISHATI

- Kamishna wa Umeme asema Serikali itaendelea kuwawezesha vijana wabunifu katika teknolojia ya matumizi bora ya nishati
- Wabunifu wa kike wapongezwa kujitokeza kwa wingi matumizi bora ya nishati nchini




Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga amekabidhi ruzuku hiyo akimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhandisi Felchesmi Mramba katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (EU) na Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP), imetoa ruzuku ya jumla ya Shilingi milioni 250 kwa wabunifu kumi waliofanya vizuri katika Mashindano ya Ubunifu na Ufanisi wa Matumizi Bora ya Nishati.

Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu kutoka Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga amekabidhi ruzuku hiyo akimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhandisi Felchesmi Mramba katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Hafla hiyo imewakutanisha wabunifu mbalimbali waliobobea katika nyanja ya ufanisi wa matumizi bora ya nishati katika maeneo matatu ambayo ni ubunifu kwenye vifaa vinavyotumia umeme kidogo, ubunifu kwenye miundombinu ya majengo yanayotumia umeme kidogo pamoja na ubunifu wa vifaa vinayoonesha matumizi ya umeme.




Picha ya Pamoja ya viongozi mbalimbali katika hafla ya utoaji wa ruzuku ya jumla ya Shilingi milioni 250 kwa wabunifu kumi waliofanya vizuri katika Mashindano ya Ubunifu na Ufanisi wa Matumizi Bora ya Nishati jijini Dar es salaam.

Mhandisi Luoga amefafanua kuwa wabunifu waliojitokeza kushindanishwa walikuwa wengi lakini baada ya uchambuzi wa kina kufanyika jumla ya washindi 10 walipatikana.

Mha.Luoga ametanabaisha kuwa katika jitihada za kuhamasisha matumizi bora ya nishati nchini, serikali ilishazindua mikakati mbalimbali ya kitaifa ikiwemo Mkakati wa Taifa wa Matumizi Bora ya Nishati pamoja na Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano kuhusu Nishati Safi ya Kupikia.

Amesema lengo kuu la mikakati hiyo ni kuchochea matokeo chanya ya matumizi bora ya nishati kwa kuzingatia ubunifu unaofanywa na vijana katika kuendeleza teknolojia zinazochangia ustawi wa sekta ya nishati nchini.

Aidha, Mhandisi Luoga amebainisha kuwa kuongezeka kwa ubunifu wa vifaa vinavyotokana na matumizi bora ya nishati kutachangia mafanikio makubwa kwa taifa hasa katika kuimarisha upatikanaji wa nishati endelevu na rafiki kwa mazingira.

“Serikali itaendelea kuwafuatilia na kuwaunga mkono vijana wabunifu katika teknolojia ya matumizi bora ya nishati kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo, ikiwemo Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB)”amesema Mhandisi Luoga

Katika hatua nyingine, amebainisha kuwa Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Nishati, imeishauri UNDP kusaidia katika kuweka mifumo ya matumizi bora ya nishati katika majengo ya Serikali yaliyo Mji wa Serikali wa Mtumba.

Hatua hiyo inalenga kuonesha mfano wa matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira katika taasisi za umma, sambamba na kuhamasisha matumizi bora ya nishati kwa ufanisi katika maeneo mengine ya Serikali.

Kwa upande wake, Naibu Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), John Rutere amesisitiza umuhimu wa ubunifu wa ndani katika kuharakisha maendeleo ya jamii na kuimarisha mabadiliko ya nishati nchini Tanzania.

“ Ninawapongeza wabunifu wa kike waliokuwa miongoni mwa washiriki wa mashindano ya ubunifu wa matumizi bora ya nishati kwani ushiriki wao unaonyesha ongezeko la ushirikishwaji wa wanawake katika sekta ya nishati na maendeleo ya taifa kwa ujumla” amesema Rutere

Ameeleza kuwa hatua ya kuwawezesha na kuinua wabunifu, hususan wanawake, itaendelea kupewa kipaumbele ili kuhakikisha teknolojia bunifu za matumizi bora ya nishati zinaibuliwa kwa kasi katika mataifa mbalimbali ya Afrika.

# WATUMISHI WIZARA YA NISHATI WAPATIWA ELIMU YA MATUMIZI SAHIHI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

- Ni baada ya Dkt.Biteko kuwakabidhi majiko yanayotumia umeme kidogo (Induction Cookers)
- Yaelezwa kuwa majiko hayo yanatumia umeme kidogo kwa gharama ndogo



Namna jiko janja la umeme linavyoonekana nakutumia wastani wa nusu uniti hadi uniti moja na nusu kwa wastani wa dakika 15 mpaka dakika 90 sawa na shilingi 65 mpaka shilingi 534

Watumishi wa Wizara ya Nishati wamepata elimu ya matumizi bora na sahihi ya majiko yanayotumia umeme kidogo ( Induction cookers) baada ya kukabidhiwa majiko hayo na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko hivi karibuni.

Dkt. Biteko aliwakabidhi majiko hayo Watumishi wa Wizara ya Nishati ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia na kwa kutambua kuwa Watumishi hao ni mabalozi katika utoaji wa elimu ya Nishati Safi ya Kupikia kwa wananchi.

Mafunzo hayo ambayo yamefanyika katika Ofisi za Wizara ya Nishati- Mtumba, Dodoma yameandaliwa na Kitengo cha Nishati safi ya kupikia kwa kushirikiana na wataalam kutoka Kampuni ya Positive Cooker.

Akitoa elimu ya matumizi bora na sahihi ya majiko hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Positive Cooker, Ndg. Atukuzwe Willson ameeleza kuwa lengo la utoaji wa mafunzo hayo ni sehemu ya uhamasishaji wananchi kutumia umeme kwa matumizi ya kupikia kupitia majiko janja yanayotumia umeme kidogo.
.

“Lengo la kutoa elimu hii ni kuhakikisha kila Mtanzania anaachana na matumizi ya nishati isiyosafi ili kulinda mazingira pamoja na afya zetu lakini pia ni sehemu ya jitihada za kuunga mkono kampeni ya nishati safi ya kupikia ambapo hadi kufikia mwaka 2034 asilimia 80 ya watanzania wanapaswa kutumia nishati safi ya kupikia.” Amesema Willson

Akizungumza kuhusu majiko hayo janja ya umeme amesema yanatumia wastani wa nusu uniti hadi uniti moja na nusu kwa wastani wa dakika 15 mpaka dakika 90 sawa na shilingi 65 mpaka shilingi 534 tu hali inayothibitisha ufanisi wa majiko hayo kuwa na gharama nafuu, kuokoa muda, kulinda afya pamoja na mazingira.



Watumishi wa Wizara ya Nishati wakipatiwa elimu ya matumizi bora na sahihi ya majiko yanayotumia umeme kidogo ( Induction cookers) baada ya kukabidhiwa majiko hayo na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko hivi karibuni.

# WATAALAM WA UFUATILIAJI NA TATHMINI WIZARA YA NISHATI WASHIRIKI KONGAMANO LA KITAIFA LA UFUATILIAJI NA TATHMINI

- Linalenga kuongeza Uwajibikaji katika Taasisi za Umma na Binafsi

Wataalam kutoka Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini Wizara ya Nishati wakiongozwa na Mkurugenzi wa Kitengo hicho Bi. Anitha Ishengoma, wameshiriki Kongamano la Nne la Kitaifa la Wiki ya Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza linalofanyika jijini Mwanza.

Kongamano hilo limewakutanisha wataalam wa ufuatiliaji na tathmini kutoka Serikalini, Sekta binafsi na Washirika wa Maendeleo.

Lengo kuu la Kongamano hilo ni kujengeana uwezo na kujadili mbinu bora zitakazosaidia kuimarisha utekelezaji wa afua za maendeleo na kuongeza uwajibikaji katika sekta za umma na binafsi.

Kongamano hilo pia linatarajiwa kuchochea mabadiliko chanya katika namna ambavyo taasisi mbalimbali nchini zinavyotekeleza na kufuatilia miradi ya maendeleo huku msisitizo ukiwa katika kujenga utamaduni wa ufuatiliaji na tathmini katika shughuli za Serikali.

Kaulimbiu ya Kongamano hilo ni "Kuimarisha Uwezo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Jamii ili Kuwezesha Utendaji Bora na Maendeleo Endelevu."

Kongamano hilo limezinduliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa.



Picha ya Pamoja ya Wataalamu kutoka Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini Wizara ya Nishati kwenye kongamano la kitaifa la wiki ya Ufuatiliaji lenye Kaulimbiu ya Kongamano hilo ni "Kuimarisha Uwezo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Jamii ili Kuwezesha Utendaji Bora na Maendeleo Endelevu."


Wataalam kutoka Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini Wizara ya Nishati katika Kongamano la Nne la Kitaifa la Wiki ya Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza lililofanyika jijini Mwanza.

# MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA YAONGEZEKA NCHINI

- Mhandisi Mramba asema yamefikia asilimia 20.3 kutoka asilimia 6.9 ya mwaka 2021
- Lengo ni kufikia asilimia 80 ifikapo 2034
- Apongeza juhudi za Rais Samia katika kuwezesha upatikanaji wa nishati safi, salama na nafuu kwa Watanzania



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha.Felchesmi Mramba akieleza namna matumizi ya nishati safi ya kupikia yalivyoongezeka nchini kutoka asilimia 6.9 mwaka 2021 hadi asilimia 20.3 huku lengo likiwa ni kufikia asilimia 80 ndani ya miaka 10, ambapo hadi sasa imebakia miaka 9.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha.Felchesmi Mramba ameeleza kuwa matumizi ya nishati safi ya kupikia nchinj yameongezeka kutoka asilimia 6.9 mwaka 2021 hadi asilimia 20.3 huku lengo likiwa ni kufikia asilimia 80 ndani ya miaka 10, ambapo hadi sasa imebakia miaka 9.

Mha. Mramba ameyasema hayo jijini Dar es Salaam wakati akizindua Kongamano la Nishati Safi ya Kupikia lililoandaliwa na kampuni ya Mwananchi kwa ushirikiano na Wizara ya Nishati pamoja na wadau mbalimbali likibebwa na kaulimbiu ya 'Nishati safi ya Kupikia Okoa Maisha, Linda Mazingira.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mha. Mramba amesema "Nishati Safi ya Kupikia siyo jambo la kinadharia bali ni jambo linalohusu maisha, mazingira na uchumi huku msingi wake mkuu ukiwa ni kulinda afya, mazingira pamoja na maendeleo jumuishi."

Aidha, Mhandisi Mramba ameendelea kuwahamasisha wananchi kutumia nishati safi ya kupikia akikumbusha kuwa, takwimu zinaonesha kuwa takribani watanzania 33,000 hupoteza maisha kila mwaka kutokana na magonjwa ya mfumo wa kupumua ambayo kwa kiasi kikubwa huchangiwa na uvutaji wa moshi unaotokana na matumizi ya nishati isiyo safi ikiwemo kuni na mkaa.

Ameeleza kuwa kutokana na athari hizo Serikali chini ya uongozi wa Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia 2024–2034 uliozinduliwa mwezi Mei 2024 ambao utawezesha asilimia 80 ya Watanzania kutumia nishati safi ya kupikia.

Sanjari na hayo, Mha. Mramba amemshukuru Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ni kinara wa nishati safi ya kupikia kitaifa na kimataifa kwa Uongozi wake wa mfano na dhamira yake ya dhati ya kuhakikisha kila Mtanzania anatumia nishati safi, salama na nafuu ya kupikia.




Picha ya Pamoja ya viongozi mbalimbali waliohudhuria katika uzinguzi wa Kongamano la Nishati Safi ya Kupikia lililoandaliwa na kampuni ya Mwananchi kwa ushirikiano na Wizara ya Nishati pamoja na wadau mbalimbali likibebwa na kaulimbiu ya 'Nishati safi ya Kupikia Okoa Maisha, Linda Mazingira.

# SERIKALI YA AUSTRIA KUFADHILI MIRADI YA UMEME TANZANIA

- Ni inayozalisha umeme kutokana na Jua; Takataka
- Ufadhili huo ni kupitia Benki ya UniCredit ya Austria
- Serikali ya Tanzania yaahidi ushirikiano

Serikali ya Austria kupitia Benki ya UniCredit imeahidi kuipatia fedha Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kiasi cha Euro Milioni 20 sawa na takribani Shilingi bilioni 60 kwa ajili ya Utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia jua na takataka.

Hayo yamesemwa na Afisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Merl Solar Technologies GmbH, Mha. Hannnes Merl alipofanya mazungumzo na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba pembeni ya Mkutano Mkuu wa 69 wa Shirika la Kimataifa la nguvu za Atomic unaoendela Jijini Vienna, Austria.

Ili kuanza utekelezaji wa miradi hiyo, Mhandisi Mramba ameikaribisha kampuni hiyo nchini Tanzania ili kukutana na wataalam na kuanza kufanya maandilizi stahiki ya miradi hiyo mipya ya kuzalisha umeme huku akiahidi kutoa ushirikiano katika kufanikisha Utekelezaji wa miradi hiyo.

Mha. Felchesmi Mramba ameeleza kuwa kampuni ya Merl imeshatekeleza miradi mbalimbali ya umeme wa jua nchini akisema "kampuni hii imetekeleza miradi ya umeme katika vijiji kumi (10) katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2017".

Ametaja miradi hiyo kuwa ni ya makontena 14 ya kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua katika Wilaya za Kongwa mkoani Dodoma, Mlele mkoani Katavi, pamoja na Uyui mkoani Tabora ambapo mradi huo uligharimu kiasi cha shilingi bilioni 16.2.



Ameongeza kuwa miradi hiyo imewezesha kuzipatia umeme nyumba na makazi 812, nyumba za Ibada 27, Shule 6 na Vituo vya Afya 8.

Mha. Mramba ameishukuru Serikali ya Austria kwa kutekeleza miradi hiyo kwa ufanisi pamoja na nia ya Serikali ya Austria kuendeleza ushirikiano na Serikali ya Tanzania katika utekelezaji wa Mkakati Mahususi wa Nishati (National Energy Compact) unaolenga kupeleka umeme kwa watanzania wote ifikapo mwaka 2030 kupitia mpango wa misheni 300.

Kikao kati ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Kampuni ya Merl kimefanyika katika Ofisi za Ubalozi wa Tanzania Mjini Vienna nchini Austria na kuhudhuriwa na Balozi wa Tanzania na Mwakilishi wa Kudumu nchini Austria Balozi. Naimi S. Aziz pamoja na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mha. Innocent Luoga.

# DKT. MATARAGIO: MRADI WA TAZA NI UTEKELEZAJI WA MPANGO MAHSUSI WA NISHATI (MISSION 300)

- Kuunganisha Tanzania na nchi zinazoizunguka
- Mikoa ya nyanda za Juu ikiwemo Mbeya, Iringa na Rukwa kunufaika
- Ameshukuru Mashirika kwa uwekezaji na kudumisha mashirikiano katika sekta ya Nishati



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Dkt.James Mataragio katika kikao cha Wadau na wawezeshaji wa utekelezaji wa mradi wa TAZA (Implementation Support Mission) katika Ofisi za Wizara ya Nishati Jijini Dar es Salaam.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Dkt.James Mataragio amesema kuwa utekelezaji wa Mradi wa TAZA unachangia kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa Mpango Mahususi wa Nishati (MISSION 300) uliokubaliwa katika Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika.

Pia umekua chanzo kikubwa cha maendeleo katika Sekta ya Nishati Tanzania na miradi mingine ya maendeleo nchini.

Dkt. Mataragio ameyasema haya wakati wa kikao cha Wadau na wawezeshaji wa utekelezaji wa mradi wa TAZA ( implementation Support Mission) katika Ofisi za Wizara ya Nishati Jijini Dar es Salaam.

Ameeleza Kuwa mpango wa Serikali ya Tanzania ni kuanzisha miradi ya kuzalisha Umeme itakayounganisha Tanzania na nchi jirani za Kenya, Zambia, Uganda, Rwanda, Burundi,



Picha ya Pamoja ya viongozi mbalimbali waliohudhuria kikao cha wadau na wawezeshaji wa utekelezaji wa mradi wa TAZA.

Msumbiji, Nchi ya Demokrasia ya Kingo(DRC) pamoja na Malawi.

Dkt. Matarajio ameendelea kusisitiza kuwa Mradi huo ni Muhimu kwa nchi yetu kwakuwa utekelezaji wake utaiwekaTanzania katika nafasi Kubwa zaidi Katika utekelezaji wa Miradi ya Umeme.

Amefafanua kuwa mradi wa TAZA utaongeza nguvu na uwezo wa kusafirisha umeme nchini kupitia Iringa-Kisada-Mbeya-Tunduma-Sumbawanga na kufikia 1,700MV umeme ambao utakao safirishwa.

Aidha, Serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) inatekeleza mradi wa TAZA (Tanzania-Zambia Transimission Interconnection Project) ambao utaunganisha Umeme kupitia Gridi za Taifa nchini Tanzania na nchi jirani ya Zambia.

Amewashukuru wawezeshaji hao kwa kuendelea kuwekeza nchini na kudumisha mashirikiano katika sekta ya Nishati Tanzania kwakuwa kumekuwa na mchango mkubwa na maendeleo endelevu ya kiuchumi nchini.

Kikao hicho kiliwashirikisha Wadau wanao wezesha utekelezaji wa Mradi huo unaosimamiwa na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Nishati na kuwezeshwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo (International Development Association ( IDA), Benki ya Dunia (WB) , Shirika la Maendeleo la Ufarans (AFD), na Umoja wa Ulaya (EU).

Kwa upande wa Mtaalamu wa Nishati kutoka Benki ya Dunia Dkt. Rhonda Jordan Antoine amesema kuwa " Benki ya Dunia inaendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania ili kuwezesha upatikanaji wa fedha za miradi ambayo ni kichocheo cha maendeleo katika jamii na hatua mojawapo ya utekelezaji wa mpango mahususi wa Nishati-Mission 300."

Dkt. Antoine amefafanua zaidi kuwa Mradi wa TAZA unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme umbali wa jumla ya kilometa 616 pamoja na vituo vya kupoza umeme katika mikoa ya Iringa-(Kisada) Kilometa 106, Mbeya Kilometa 185, Mbeya -(Tunduma) Kilometa 122 pamoja na1 mradi wa kusafirisha Umeme Rukwa - (Simbawanga) wenye urefu wa kilometa 203.

# MFUMO WA UFUATILIAJI NA TATHMINI NI NYENZO YA UTENDAJI KAZI FANISI SERIKALINI- DKT. BITEKO

- Awaasa Maafisa Ufuatiliaji na Tathmini kutokuwa waoga wanapotekeleza majukumu kwa maslahi ya Taifa
- Ataka kazi za Ufuatiliaji na Tathmini ziongozwe na Uaminifu, Uadilifu
- Afunga Kongamano la Kitaifa la Ufuatiliaji, Tathmin na Kujifunza



Mkuu wa Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini (M&E) kutoka Wizara ya Nishati, Bi. Anitha Ishengoma, akielezea kuwa Wizara imejipanga kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathimini ili kuboresha upatikanaji wa nishati ya uhakika na nafuu kwa Watanzania.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amehitimisha Kongamano la Nne la Kitaifa la Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza lililofanyika Jijini Mwanza akiweka mkazo kuwa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha kuwa kila taasisi inatimiza wajibu wake kwa ufanisi na hivyo kufikisha huduma bora kwa wananchi.

Kutokana na hilo, Dkt. Biteko amewataka Wataalam wa Ufuatiliaji na Tathmini nchini kufanya kazi kwa uaminifu na uadilifu bila kuogopa kuchukiwa kwani taifa linawategemea ili kuweza kutoa huduma bora kwa wananchi.

"Hakuna mtu au taasisi inayoweza kufanikisha majukumu yake bila kufanya tathmini, ninyi ndio mnaoweza kutambua changamoto mapema na kuzitafutia suluhisho kabla hazijawa kubwa, taasisi yoyote inayokosa mfumo huu inafanana na timu inayoingia uwanjani bila refa.." Amesema Dkt. Biteko

Ametoa mfano kuwa katika sekta ya umeme, kabla ya kupeleka huduma hiyo eneo lolote lazima tathmni ifanyike ili kuepuka kurudia kazi mara mbili na pia




Picha ya Pamoja viongozi mbalimbali katika Kongamano la Nne la Kitaifa la Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza lililofanyika Jijini Mwanza akiweka mkazo kuwa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha kuwa kila taasisi inatimiza wajibu wake kwa ufanisi na hivyo kufikisha huduma bora kwa wananchi.

tathmini husaidia kuona matokeo ya huduma husika kwa wananchi.

Kuhusu Kongamano hilo, Dkt. Biteko ameeleza kuwa mwaka jana lilihudhuriwa na washiriki 900 huku mwaka huu likivutia washiriki 1,300.

Kwa upande wake Mkuu wa Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini (M&E) kutoka Wizara ya Nishati, Bi. Anitha Ishengoma, amesema Wizara imejipanga kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathimini ili kuboresha upatikanaji wa nishati ya uhakika na nafuu kwa Watanzania.

Ishengoma amesema Sekta ya Nishati inahusisha taasisi kubwa sita pamoja na kampuni tanzu tano ambapo kila robo mwaka Wizara hufanya vikao vya kujadili tathmini ya utendaji kazi wa Wizara na Taasisi zake vinavyoongozwa na Waziri ili kujadili masuala mbalimbali kuhusu tathmini ya utendaji kazi ikiwemo kubainisha maeneo yenye changamoto zinazojitokeza na kuweka mikakati ya kuboresha utendaji kazi.

Kongamano la Ufuatiliaji na Tathmini limewakutanisha wadau kutoka Taasisi za Umma na Sekta Binafsi kwa lengo la kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini kwa maendeleo endelevu.

# UTENDAJI KAZI WA WIZARA YA NISHATI NA TAASISI ZAKE WAIMARIKA

- Wapanda kutoka asilimia 95 hadi 96.16 katika kipindi cha robo mwaka
- Mhandisi Mramba asema ongezeko hilo linaakisi utoaji wa huduma kwa wananchi
- Apongeza Taasisi kuendelea kuboresha utoaji huduma kwa Wananchi
- Asisitiza mitandao ya kijamii kutumika ipasavyo utoaji elimu Nishati Safi ya kupikia




Picha ya Pamoja ya Viongozi mbalimbali wa Wizara ya Nishati katika kikao cha Tathimini ya utendaji kazi iliyofanywa na kitengo cha Ufuatiliaji na tathimini kwa kipindi cha robo 2024/2025.

Imeelezwa kuwa, utendaji kazi wa Wizara ya Nishati kupitia Taasisi inazosisimamia umezidi kuimarika na kufikia asilimia 96.16 katika kipindi cha robo nne ya mwaka 2024/2025.

Hayo yamefahamika wakati wa kikao cha Tano cha Tathmini ya utendaji kazi wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa robo nne ya mwaka 2024/2025 kilichofanyika jijini Dodoma na kuongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mhandisi Felchesmi Mramba.

Tathmini hiyo ya utendaji kazi iliyofanywa na Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini katika Wizara ya Nishati imeonesha kuwa katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2024/2025 utendaji kazi wa Taasisi zilizochini ya Wizara ya Nishati umeimarika kwa zaidi ya asilimia 96 kutoka asilimia 95 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2024/2025.

Kufuatia tathmini hiyo, Mha. Mramba amewapongeza Watendaji wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa kuendelea kuboresha utendaji kazi kupitia utekelezaji wa miradi na utoaji huduma kwa wananchi hali inayoleta matokeo chanya katika Sekta ya Nishati.

"Tathmini hizi zinaakisi kile tunachokitekeleza kwani huduma zimeendelea kuboreshwa pamoja na kuimarika zaidi, sisi kama Wizara tumeendelea kuhakikisha kuwa tunatoa huduma bora kwa wananchi".Ameeleza Mha. Mramba

Katika kikao hicho, Mha.

Mramba amelipongeza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa kuendelea kutoa taarifa kwa wananchi kwa wakati jambo ambalo limeleta ongezeko la kuimarika kwa utoaji huduma.

Aidha, kuhusu Nishati Safi ya Kupikia, amesisitiza kutumia mitandao ya kijamii katika kuitangaza nishati hiyo hususani matumizi ya majiko yanayotumia umeme kidogo akieleza kuwa mitandao ya kijamii inanguvu kubwa ya kufikisha habari kwa



Picha ya Pamoja ya Viongozi na wadau wa mbalimbali wa Nishati katika kikao cha Tathimini ya utendaji kazi iliyofanywa na kitengo cha Ufuatiliaji na tathimini kwa kipindi cha robo kilichofanyika jijini Dodoma.

watu wengi na kwa muda mfupi lengo likiwa ni kutimiza adhma ya Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kuwa wananchi wanahama kutoka matumizi ya Nishati isiyo safi ya kupikia kwenda kwenye matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia.

Vilevile, amekipongeza Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini cha Wizara ya Nishati kwa kutekeleza jukumu lao kwa ufanisi huku akisisitiza kuwa Kitengo hicho kipewe ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuhakikisha Idara, Vitengo na Taasisi zinawasilisha taarifa za utendaji kazi kwa wakati ili kitengo hicho kiongeza ufanisi zaidi katika kazi ya tathmini na hivyo kuboresha utendaji kazi.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio amezipongeza Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Nishati pamoja na Idara na Vitengo vya Wizara ya Nishati kwa utendaji kazi wenye kuleta matokeo chanya kama ambavyo tathmini ya utendaji kazi ilivyoonesha kuwa ufanisi wa kazi umeendelea kuboreshwa na kuimarika zaidi.

Awali, Akiwasilisha taarifa ya tathmini ya utendaji kazi kwa Wizara na Taasisi zake, Mkurugenzi wa Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini, Wizara ya Nishati, Bi. Anita Ishengoma alisema kuwa kutoka zoezi la tathmini lianze kufanyika, limeleta ufanisi hasa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali pamoja na mipango ya Wizara kwani utendaji kazi wa Taasisi umeongezeka.

Amesema kuwa Idara/Vitengo zilizofanya vizuri zaidi katika tathmini iliyofanyika katika Wizara ya Nishati kwa kipindi cha robo nne ya mwaka 2024/2025 ni Idara ya Umeme na Nishati Jadidifu (nafasi ya kwanza), Kitengo cha Manunuzi -(Nafasi ya Pili) na - Kitengo cha Tehama ( Nafasi ya Tatu).

Aidha, Taasisi zilizofanya vizuri zaidi katika utendaji kazi kwa tathmini iliyofanyika katika kipindi cha robo nne ya mwaka 2024/2025 ni Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) - nafasi ya kwanza), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) -nafasi ya Pili) na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA)- nafasi ya Tatu).

Mikoa ya Kitanesco iliyofanya vizuri katika utendaji kazi kwa tathmini iliyofanyika katika kipindi cha robo nne ya mwaka 2024/2025 ni Manyara (nafasi ya kwanza), Kinondoni Kusini ( nafasi ya Pili) na Simiyu ( nafasi ya Tatu).

Ilielezwa kuwa utendaji kazi wa mikoa ya kitanesco kwa ujumla umeimarika kwani hamna mkoa ambao utendaji wake umekuwa chini ya asilimia 91.83.

Katika Kikao hicho pia Taasisi ziliweza kuwasilisha taarifa za utendaji kazi wake. Kikao hicho kilihudhuriwa na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, Wakurugenzi wa Vitengo Ufuatiliaji na Tathmini kutoka Wizara mbalimbali, Menejimenti ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake pamoja na Mameneja wa Kanda wa TANESCO.

# UJENZI MRADI WA TAZA WAFIKIA ASILIMIA 58 KWA UPANDE WA TANZANIA

- Nguzo 420 za kusafirisha umeme wa kV 400 zasimikwa
- Benki ya Dunia yaipongeza Tanzania kwa kasi ya utekelezaji wa mradi
- Wakandarasi waishukuru Serikali kutoa fedha kwa wakati



Wataalamu mbalimbali walipo tembelea Ujenzi wa mradi wa usafirishaji umeme wa msongo wa kilovoti 400 unaounganisha Tanzania na Zambia (TAZA) umefikia asilimia 58 ya uekelezaji wake kwa upande wa Tanzania.

Ujenzi wa mradi wa usafirishaji umeme wa msongo wa kilovoti 400 unaounganisha Tanzania na Zambia( TAZA) umefikia asilimia 58 ya uekelezaji wake kwa upande wa Tanzania.

Hayo yameelezwa na Mwakilishi wa Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Sadick Mwaifunga wakati wa ziara ya ukaguzi na tathmini ya utekelezaji wa mradi huo inayohusisha watendaji wa Wizara ya Nishati, Shirika la Umeme Tanzania ( TANESCO) pamoja na Benki ya Dunia(WB).

Ziara hiyo imehusisha ukaguzi wa mradi katika mikoa ya Iringa, Mbeya na Rukwa kwa kukagua ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Kisada- Iringa, Iganjo-Mbeya hadi kituo cha kupoza umeme cha Malangali Sumbawanga yenye urefu wa Kilometa 616 pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme Katika mikoa hiyo.

"Mpaka sasa utekelezaji wa mradi unaendelea vizuri na sasa umefikia asilimia 58 ikihusisha ujenzi wa miundombinu ya njia kusafirisha umeme pamoja vituo vya kupoza umeme" Amesema Mhandisi Mwaifunga

Amefafanua kuwa, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Iringa - Kisada; Kisada - Mbeya; Mbeya - Tunduma na Tunduma - Sumbawanga umefikia asilimia 81.

Pia ujenzi wa vituo vya kupoza umeme Iringa, Kisada, Mbeya, Tunduma na Sumbawanga umefikia asilimia 35.

Mha. Mwaifunga amesema katika Mradi huo jumla ya nguzo 1614 za umeme wa kV 400 zitajengwa kwa urefu wa Kilometa 616.

Aidha, ameeleza kuwa hadi sasa tayari zaidi ya nguzo 420

zimeshasimikwa na zoezi hilo linaendelea.

Kwa Upande wake Msimamizi wa Mradi huo kutoka Shirika la Umeme Tanzania(TANESCO), Mhandisi Elias Makunga amewataka wakandarasi kuongeza kasi ya ujenzi wa mradi huo ili kukabiliana na changamoto ya hali ya hewa hasa nchi inapoelekea katika kipindi mvua.

Amesema wakandarasi wanamuda mwingi wa kufanya kazi kipindi cha kiangazi hivyo watumie kipindi hicho kufidia Kazi zitakazosimama wakati wa kipindi cha mvua.

“ Hatutamani kuona mkandarasi anasingizia mvua kuwa imekwamisha utendaji wake wa kazi, ni vyema sasa kipindi hiki cha kiangazi kazi zifanyike kwa kasi kubwa ili kutocheleweshа mradi huu unaosubiriwa kwa hamu kubwa” amesisitiza Mha. Makunga

Benki ya Dunia kwa upande wake imeipongeza Wizara ya Nishati kwa kusimamia vyema mradi huo hasa kwa hatua nzuri ya utekelezaji wa mradi.

Kwa upande wake Meneja Mradi kwa upande wa Mkandarasi anayetekeleza ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Kisada Iringa hadi Mbeya, Mhandisi Ananthan Pannerselvam ameishukuru Serikali kwa kuendelea kutoa fedha kwa wakati za kutekeleza miradi huo.

Amesema kuwa utekelezaji wa mradi unaendelea vizuri na mpaka sasa hakuna changamoto yoyote inayoweza kuhatarisha utekelezaji ambapo ameahidi kukamilisha kazi kwa wakati.



Picha ya Pamoja katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Kisada- Iringa, Iganjo-Mbeya hadi kituo cha kupoza umeme cha Malangali Sumbawanga yenye urefu wa Kilometa 616 pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme Katika mikoa hiyo.

# DKT. BITEKO AHIMIZA WANAMICHEZO KUCHUNGUZA AFYA ZAO

- Tasnia ya Burudani na Michezo kwa mwaka 2024/2025 imekuwa kwa asilimia 18
- Watumishi 3,353 washiriki SHIMIWI mwaka 2025
- Awahimiza washiriki SHIMIWI kusikiliza kampeni za wagombea na kupiga kura Oktoba 29
- Serikali kujenga Kituo cha Kulea Vipaji Mwanza



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akitoa rai kwa wanamichezo kufanya uchunguzi wa afya zao kwa kuhusisha vipimo vyote muhimu ikiwemo vya moyo, damu na viungo vyote vya mwili ili kuhakikisha usalama wa Afya zao.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko ametoa rai kwa wanamichezo kufanya uchunguzi wa afya zao kwa kuhusisha vipimo vyote muhimu ikiwemo vya moyo, damu na viungo vyote vya mwili ili kuhakikisha usalama wa Afya zao.

Ameliomba Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali Tanzania (SHIMIWI) kuendelea kushirikiana na Taasisi za Afya nchini na kuweka mfumo sahihi wa upimaji wa afya kwa wanamichezo.

Dkt. Biteko ametoa rai hiyo katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza wakati akifungua rasmi mashindano ya 39 ya SHIMIWI yaliyotanguliwa na maandamano ya watumishi wa umma.

Ametaja masuala mengine muhimu ya kuzingatiwa kwa wanamichezo " Mazoezi ya awali na mbinu nyingine mbalimbali kwa kujenga uimara wa mwili kupitia mazoezi kama vile kukimbia, mazoezi ya nguvu na mazoezi mfano wa hayo. Pia, kuiandaa akili ili kuikabili michezo na mashindano kwa ujumla, wataalamu husema mafanikio huanza katika fikra," amesema Dkt. Biteko.

Ameongeza kwa kusema Nimejulishwa kwamba, katika michezo ya mwaka wa jana mlisajili watumishi 2,995. Na mwaka huu 2025 mmesajili watumishi 3,353 kushiriki michezo hii ambapo ni sawa na ongezeko la asilimia 12 hongereni sana,"

Pia, ameipongeza Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na viongozi wa SHIMIWI kwa kazi kubwa ya kuratibu, kusimamia na kuendeleza michezo nchini.

Dkt. Biteko pia amewataka waajiri kutekeleza maagizo ya Rais Samia ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya watumishi wanaoshiriki SHIMIWI huku akiwaeleza watumishi kuwa Rais Samia anawatakia kila la heri katika



michezo yao na kuwa yuko tayari kuendelea kushirikiana nao ili kupata mahitaji yao.

Amesema takwimu zinaonesha kuwa, Tasnia ya Burudani Tanzania ambayo michezo ipo ndani yake imeendelea kukua kwa kasi na kuchangia sehemu muhimu katika Pato la Taifa na kuongeza ajira nchini.

Ametolea mfano kwa mwaka 2022/2023 sekta hiyo imekua kwa asilimia 15 na mwaka 2023/24 kwa asilimia 18. Aidha, uwepo wa watumishi wanaoshiriki SHIMIWU zaidi ya 3,000 Jijini Mwanza umesaidia kutengeneza ajira na kuchangia mzunguko wa fedha.

“Nawaomba viongozi muweke mikakati ya kuhakikisha manufaa haya yanawagusa Watanzania wa maeneo yote nchini kwa maslahi mapana ya Taifa kwa ujumla,” amesisitiza Dkt. Biteko.

Halikadhalika amewaasa wachezaji wote kujenga fikra ya kupendana na si kuchukiana baina yao pamoja na kufuata na kuzingatia taratibu zote za michezo.

Fauka ya hayo, Dkt. Biteko amewasihi wanamichezo hao kuhimizana kushiriki kwa amani katika zoezi la kusikiliza kampeni za wagombe na kukumbushana umuhimu wa kupiga kura.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Said Mtanda ameishukuru Serikali ya Rais Samia kwa kuendelea kuwekeza katika michezo ambapo inajenga Kituo cha Kulea Vipaji katika Chuo cha Michezo Malya.

Pia, amesema shughuli za kampeni mkoani humo zinaendelea vizuri na Oktoba 29, 2025 wananchi watajitokeza kwa wingi kupiga kura.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa amemshukuru Rais Samia kwa kuendelea kuruhusu kufanyika kwa mashindano ya SHIMIWI kwa watumishi wa umma kwa miaka mitano mfululizo kwa kuwa yameendelea kuwa na faida kubwa.

“ Wizara yetu itaendelea kuhakikisha michezo hii inafanyika kwa haki, sisi kama Wizara tunamshukuru Mhe. Rais kwa maelekezo yake na kutoa raslimali fedha ili kukuza sekta ya michezo nchini,” amesema Msigwa.

Ametaja jitihada za Serikali katika kuimarisha sekta ya michezo ni pamoja na kukamilisha viwanja na shule za michezo katika maeneo mbalimbali nchini.

Ameongeza kuwa Tanzania imeendelea kufanya vizuri katika michezo kimataifa katika ngazi mbalimbali.
Ameongeza kuwa Tanzania imeendelea kufanya vizuri katika michezo kimataifa katika ngazi mbalimbali.

Katika salamu zake za utangulizi, Mwenyekiti wa SHIMIWI, Daniel Mwalusamba amesema Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Baraza la Michezo la Taifa imefanya shughuli zake kwa ufanisi mkubwa na hivyo kuleta matokeo chanya.

Awali, Dkt. Biteko ametembelea banda la Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ambapo ameelezwa majukumu na huduma zinazotolewa kwa wananchi.

Mashindano ya Michezo ya 39 ya SHIMIWI kwa mwaka 2025 yanayoongozwa na kaulimbiu “ Michezo kwa Watumishi Huongeza Tija Kazini, Jitokeze Kushiriki Uchaguzi Mkuu 29 Oktoba 2025 kwa Amani na Utulivu Kazi Iendelee.”yatafikia tamati Septemba 16, 2025.


For more info
www.nishati.go.tz
The United Republic of Tanzania
Ministry of Energy